HIASTORIA YA PAROKIA YA MSIMBAZI KUTOKA 1952

Tarehe 13.01.1952 ndio ulikuwa mwanzo wa parokia ya msimbazi. Katika mkutano wa pekee isiku ile katika ofisi ya Jimbo la Dar es Salaam, Askofu Edgar Maranta Pamoja na Muhudumu Mkuu wa Wakapuchini hapa Dar es Salaam Padre Vincent Pamoja na mapadre wengine waliweka mipaka ya Pamoja ya Msimbazi. Padre Clemence Hug aliteuliwa kuwa Paroko wa kwanza

Majengo na eneo la Parokia ya msimbazi

Kanisa;

Ujenzi wa Kanisa la msimbazi ulianza tarehe 25-09-1953 chini ya uongoziwa Bruda Frans Popp. Jiwe la Msingi wa Kanisa liliwekwa na na Askofu Mkuu Edgar Maranta tarehe 14-2-1954. Maneno juu ya jiwe la msingi yalisomeka hivi

D.O.M (DEO OPTIMO MAXIMO
ILLIBATAE IN CONCEPTU MATRI GRATI DEDICANTI AFR
1953 — 1955

Tafsiri yake;

KWA AMUNGU MKUU NA MWEMA KULIKO WOTE
Waafrika wenye shukrani wanaweka Wakfu (Kanisa Hili) kwa heshima ya Maria aliyekingiwa Dhambi ya asili
1953—1955

Kubarikiwa Kanisa;
Kanisa lilibarikiwa tarehe 12-06-1955 na Askofu Mkuu Edgar Maranta. Katika kumbukumbu iliandikwa kwamba, viti vya Kitubio vilitengenezwa Kwiro na pia imeandikwa kwamba, mtu wa kwanza kuungama alikuwa Bwana Joseph Theobald, Muhunzi ambaye alionekana sana katika eneo la Msimbazi. Askofu Maranta alimleta Mr Ponziano Togni (Mwitaliano) ambaye alichora picha ya Bikira Maria wa Fatima na Watoto Lucia Fransisko na Yasinta.
Katika kumbukumbu ya Parokia inaelezwa kuwa, Sr. Rosalina (Baldegg) alianza kazi katika sakristia katika Kikanisa cha ndani ya nyumba ya masista kutoka mwaka 1944 na mwaka 1955. Sakramenti Kuu ilihamia katika Kanisa jipya na Sista huyo aliendele na kazi hiyo hadi mwaka 1971

Shule

MsImbazi ilipoanza kuwa Parokia ilikuwa na shule ya wasichana katika nyumba ya Masista Pamoja na Bweni, chini ya Masista wa Baldegg, k.m Sr. Wiltrud na Sr Gabriela. Pia palikuwa na Bweni la wavulana ambao walikwenda kusoma shule ya serikali.

Shule ya wavulana ilijengwa mwaka1955. Bweni la wavulana lilikuwa chini ya Wakapuchini lakini ilikuwa sio rahisi kuwaongoza. Muda mwingi walikaa peke yao. Mwaka 1966 Bweni hilo lilifungwa.

Shule ya wasichana ilijengwa mwaka 1960 darasa la 14 na mwaka 1962 darasa la 5-7 mwaka 1962 serikali ilipo taifisha shule zote. Parokia ilibaki haina madaraka juu ya shule japokuwa mafundisho ya dini yaliendelea. Mpaka sasa wanafunzi wanapata vipindi vya dini mashuleni na nafasi ya kuhudhuria misa katika siku ya ijumaa asubuhi saa 1:15

Mwaka 1985 Padre Zachareus alianzisha shule ya ushonaji na shule hii ilitumia nafasi katika ukumbi. Na ilikuwa chini ya Masista wa Kilimanjaro. Mkuu wa kwanza wa shule alikuwa Sista Emeldina na mwanzoni mwa mwaka 2002 alikuwa Sr. Shija.

Ingawa Parokia ilikuwa na Vigango vyake ambavyo vilikuwa na shule mbalimbali za Watoto wadogo kutoka zamani, Padre Amandus alifaulu kuanzisha shule ya chekechea (Mtindo wa Montessor) mwaka 1973 chini ya uongozi wa Parokia. Walimu wakati hu wakiwa Sr. Emmanuela na Sr. Iriminaw a Shirika la Mgolole Morogoro

Ukumbi

Tangu mwaka 1961 Parokia ilikuwa na Msimbazi Center kama Jirani. Parokia iliweza kutumia ukumbi na madarasa kwa mikutano na shughuli nyingine , lakini mwaka 1977, parokia chini ya uongoz wa Padre Diego ilipata ukumbi wake. walianza kutumia ukumbi kwa shule ya ushonaji. Padre Ambrosi Mosha aliongeza jengo la ukumbi kwa kujenga gorofa ya pili kwaajili ya shule tu. Katika sehemu ya chini alitengeneza ofisi ambazo zilitazamiwa kuwa ofisi za Paroko na wenzake ili nyumba ya Mapadre ipate kuwa kwa kukaa mapadre tu. Lakini mpaka sasa ofisi za mapadre bado zipo katika nyumba ya Mapadre. Nyumba hii ya Mapadre ilijengwa kwaka 1959.

Halmashauri ya Parokia

Halmashauri ya Parokia Mwaka (2001- 2004) ilichukua hatu ya pekee kurekebisha ukumbi na kujenga vyoo ili Parokia iweze kukodisha ukumbi kwaajili ya mikutano , semina, tafrija na mengine kama njia ya kujiongezea mapato ya Parokia

Eneo la Msimbazi.

Jimbo la Dar es Salaam lilikuwa na eneo kubwa hapa Ilala kutoka mwanzo, lakini kwa sasa eneo limepunguzwa sana. Katika kumbukumbu imeandikwa kwamba hapo mwaka 1952 serikali ilitaka kuchukua mlima Kigogo “Mabruda waliwahi kukata miti ambayo ilikuwa mali ya misioni mwaka 1965 Waziri wa Ardhi bwana Sijaona alitangaza kwamba sehemu ya Msimbazi imechukuliwa lakini kabla ya matangazo hayo aliwahi kuonana na Askofu Maranta kuacha sehemu Fulani bado

kwa Jimbo Mabadiliko makubwa yalitokea kati mwaka 1970 – 1975. Kiwanja cha Msimbazi kilipunguzwa sana. Serikali ilihitaji nafasi kwa watu wa Buguruni. Muda huo ulikuwa muda mgumu wa kupatana na kushirikiana. Kiwanja cha Parokia ni kidogo sana sasa. Majengo mengi ambayo yanaonekana si ya Parokia, kwa mfano, Procura ya Mahenge, shule ya Montesori, San Damiano, nyumba ya Msimbazi Centre, Kijiji cha wasiojiweza eneo (plot) la Msimbazi ulijengwa na Padre Mrosso mwaka 1999 aliyekuwa Mkurugenzi wa Msimbazi Centre kwa kipindi hicho. Ukuta huo ni msaada mkubwa kwa usalama, lakini hata hivyo Msimbazi ni bado mahali ambapo watu wengi mno wanapita kuelekea makwao.

Parokia ya Msimbazi Imezaa Parokia Nyingine.

Kwa sababu ya kuongezeka kwa wakatoliki Parokia ya Msimbazi ilianza kuzaa porokia nyingiine. Magomeni mwaka 1965, Tabata mwaka 1987 na Vingunguti mwaka 1999.

Kariakoo: Kutoka Breweries mpaka Msimbazi Street ni Kigango cha Kariakoo Kikanisa kilijengea mwaka 1929/30. Wakristo wa huko walihudumiwa na Mapdre wa St. Joseph. Ingawa ni kigango cha muda mrefu hakikupata kuwa Parokia. Mpaka sasa kigango cha Kariakoo ni kati ya vigango tisa vya Parokia ya Msimbazi. Kigango hiki kinapata huduma ya Misa takatifu mbili kwa kila Jumapili.

Buguruni ilikuwa kigango kikubwa kupita vyote, jumuiya 17, Tarehe 13-3-2001 Padre Mosha alipokea barua kutoka kwa Padre Jovin Bekekere kuhusu “Kumega sehemu ya Parokia, yaani Kigango cha Kigogo B, na kuunda Kigango cha Luhanga.” Waamini hawakufurahia uamuzi huo na mpaka tarehe 13-1-2002 hatukuweza kutimiza mapendekezo hayo ya Jimbo. Ingawa Paroko Mosha na baadaye Padre Mansuetus walijua ni lazima na ni faida kwa huduma ya kichungaji, walijaribu kuwaongoza waamini kwa utaratibu.

Mwanzoni wa mwezi Desemba 1889 Wabenediktini walirudi Dar es salaam na walianza kukaa mjini. Masista walinunua viwanja zaidi na mwaka 1914 walikuwa na nyumba yao pamoja na bweni la wasichana (Kwa sasa ni nyumba ya Masista wa Mgolole). Imeandikwa katika kumbukumbu kwamba tarehe 17-5-1914 walikuwa na Misa takatifu ya kwanza katika nyumba yao. Baada ya vita kuu mwaka 1918 Masista wa Kijerumani walikuwa na shida ya kuendelea na kazi kwa sababu ya uraia wao chini ya utawala wa Waingereza. Hali hiyo iliwalazimu Wabenediktini wote pamoja na Askofu Spreiter kuondoka Tanganyika.

Mwaka 1921 Wakapuchini wa Uswissi pamoja na Masista wa Baldegg walifika Jimbo la Dar es Salaam na kati yao wengine walianza kukaa Msimbazi na kuendelea na kazi kama Wabebediktini.

Kwa upande wa kazi ya kichungaji Msimbazi ilikuwa kigango cha St. Joseph kama Kurasini, Pugu na Mbagara.

Kwa muda wa miaka 30 chumba kimoja katika nyumba ya Masista kilitumika kama kikanisa. Kila siku Padre aliadhimisha Misa Takatifu na kutoa mafundisho. Alifika kwa baiskeli kutoka St. Joseph. Jumapili masista na watoto walipanda gari la punda wakaenda kusali huko mjini. Mpango huu uliendela mpaka alipoanza kukaa Padre Clemens alipoanza kukaa Msimbazi mwaka 1944.

Makundi ya Waamini katika Parokia ya Msimbazi.

Mapadre

Maparoko:	1952 – 1956	Padre Clemens
	1956 – 1960	Padre Victorian
	1961 – 1964	Padre Wendelin
	1964 – 1967	Padre Mansuetus
	1967	Padre Paulinus
	1967 – 1975	Padre Amandus
	1975 – 1976	Padre Oswin
	1976 – 1977	Padre Diego
	1978 – 1981	Padre Leonius
	1981 – 1986	Padre Zecheus
	1986 - 1993	Padre Accursius
	1993 – 1997	Padre Zecheus
	1997 – 1999	Padre Tarimo
	1999 – 2001	Padre Mosha
	2001	Padre Mansuetus

Mapadre wengi wamekaa Msimbazi kama wasaidizi wa Maparoko, Wamisionari na Wazalendo. Kwa sababu Parokia yetu ilikabidhiwa kwa Wakapuchini, wahudumu katika Parokia hii ni Mapadre na Mabruda kutoka shirika hilo. Safari moja tu tulikuwa na Padre mmoja wa Jimbo la Bukoba kama msaidizi wa Paroko, yaani Padre John Joseph Rwechungura, mwaka 1964 -1968.

Masista

Waamini wa Msimbazi wamezoea kuwaona masista wengi kila siku Kanisani na eneo la Msimbazi, lakini wasifikiri wote ni kwa ajili ya Parokia yetu. Masista wa Baldegg ambao walifanya kazi muda mrefu [yaani kutoka mwaka 1921] hapa Parokiani, kwa siku hizi wanashughuli nyingine. Tangu

1-7-1971 Masista wa Mgolole Morogoro walianza kukaa hapa Msimbazi. Masista wa Bukoba walifika mwaka 1972, Masista wa Mahenge mwak 1972, Masista wa Msalaba Mtakatifu [Holy Cross Sisters] mwaka 1983, Masista wa Kilimanjaro mwaka 1985, na Masista wa Dada Wadogo mwaka 2001.

Makatekista

Makatekista walisaidia na wanasidia sana katika kazi ya Kiuchungaji Parokiani.

Kumbukumbu inawataja: George Hussein, Kamilius Ngawilla, John Bosco Ndungru, Marco Sangawe, fredy Shoma, Aidan Masabi na Menrad Msike. Sista Evarista [Baldeg] pia alisaidia sana kwa kutoa mafundisho kutoka 1973 – 1988. Pia masista wazalendo wengine walikuwa katika Parokia yetu kama makatekista lakini kuwataja wote ni vigumu kwa sababu ni desturi katika mashirika yao kufanya uhamisho kwa ghafla au baada ya kukaa kwa muda mfupi.

Tarehe 13-1-2001 tulikuwa na Charles Magombeka [katika Parokia yetu tangu mwaka 1984] na Martin Rutha, Sista Laud [Mgolole], Hosesta [Mgolole] Zabinus [Kilimanjaro], Anwarite [Mahenge] na Sista Fransiska [Mahenge] aliwasaidia sana watoto viziwi na bubu wa shule ya Buguruni

Walei

Walei walipewa nafasi yao kushirikiana na maendeleo ya Parokia. Inaonekana wakati wa Padre Wendelin [1964] Walei walikuwa pamoja katika CLAD yaani Baraza la Utume wa waamini wa Dar es Salaam. Mpango huo haukuridhisha. Tarehe 8 Nov. 1964 palikuwa na uchaguzi wa Parish Council au Halmashauri ya Parokia. Walitunga sheria ya Halmashauri na ilkubaliwa na Askofu Maranta kwa mwaka mmoja. Baadaye ilikuwa ni lazima kufuata katiba kadri ilivyokubaliwa na Maaskofu wa Tanzania. Tunawashukuru Walei wengi sana ambao kwa njia mbalimbali walikuwa katika Halmashauri ya Parokia na walifanya bidii kuwasaidia Mapdre katika uongozi wa Parokia.

Kadri tunavyoweza kuchota kutoka kumbukumbu, wafuatao walikuwa wenyeviti wa halmashauri ya Parokia: Stephan Mlatie, Joseph Mutayoba, Lucas Raphael, Alfons Haule, Peter Balatazar, Marcus Mahundi, Joseph Samaka, Sales Kingumwile na siku hizi Joakim Lyimo. Hapo pia tunapenda kuwataja wanachama wa vyama vya kitume ambavyo viko katika Parokia yetu na vinaimarisha hali ya Parokia kwa utakoso wa wanachama na kwa kazi ya kitume. Shirika la Moyo Mt. wa Yesu na Walegio Maria walikuwepo tangu mwanzo wa Parokia yetu Wawata, Wanaume Wakatoliki, CPT, Viwawa, Virafra, Watersiari, utume wa Fatima, Waimbaji, Watoto wa Yesu, na Mt. Monica [wajane] wote wanawashirikisha waamini wengi katika maendeleo ya Parokia.

JUMUIYA NDOGO NDOGO

Kufuatana na mapendekezo ya Maaskofu wa AMECEA kutumia Jumuiya ndogondogo kuimarisha maisha ya Kikristu, Parokia ya Msimbazi haibaki nyuma kutimiza mapendekezo hayo. Kutoka katika kumbukumbu, Parokia ilikuwa na Jumuiya 12 katika vigango vya Kigogo, Mchikichini na Sharif Shamba. Hatuna habari ni ipi ilikuwa ya kwanza. Mpaka mwaka 2002 tulikuwa na Jumuiya 29. Karibu kila siku Mapadre wa Msimbazi wanakumbushwa uwepo wa Jumuiya hizo kwa sababu karibu kila siku wanapata ombi la mazishi ya mmojawapo wa wanajumuiya. Tunategemea pia msaada wa Jumuiya kuamua juu ya ombi la ubatizo, ndoa nk. Kwa kuadhimisha Misa katika Jumuiya Mapadre wanapata nafasi ya kuwa karibu na waamini. Uhai wa Jumuiya kwa akina baba, watoto mara myingi hawana nafasi kwa sababu wanachelewa kurudi shuleni.

Matukio ya pekee:

RALLY YA ROZARI: Mwaka 1955. Mwezi mmoja baada ya kubariki Kanisa Parokia ilikuwa na watu wengi sana mbele ya kanisa kwa ajili ya Rally ya Rozari. Fr. Payton ambaye alikuwa Mtume wa pekee wa ibada ya Rozari aliwahamasisha watu kusali Rozari hasa katika familia.

MAFUNGO MAKUU: Mafungo na mafundisho ya pekee yalitolewa wakati wa Paroko Fr. Victorian tarehe 19-2-1961 hadi 5-3-1962. Mapadre kutoka majimbo mengine walifika na waliweza kuwafuata waamini wengi na kuwapa moyo wa kurkebisha maisha yao. Tarehe 5-3-1962 Msalaba Mkubwa uliwekwa katika kiwanja karibu na shule ya Wavulana kama ukumbusho wa mafungo makuu. Msalaba huo bado upo lakini umesahauliwa na unakaa kati ya nyumba za watu.

KUJENGA KIHEKALU

Mwaka 1999 Parokia iliweza kujenga mahali pa pekee kwa Bikira Maria ambapo panaitwa Kihekalu cha Bikira Maria Tarehe 15-8-1999 uzinduzi wa Kihekalu ulifanyika na Mwadhama Kadinali Pengo. Tangu siku ile Parokia inasali Rozari walau kila Jumamosi, kila siku wakati wa Mei na Oktoba na kila Sikukuu ya Maria. Zaidi ya hayo kuna kundi la waamini ambao wanafanya ibada karibu kila siku baada ya Misa ya pili asubuhi.

KUJENGA KALVARIO: Baada ya mwaka wa Jubilee [2000] Parokia ya Msimbazi ilichaguliwa na Mwanadhama Kardinali Polycalip Pengo kutunza Msalaba wa Jubilee. Karmel na wenzake walifika kutoka Uswissi na kujenga mahali pa pekee kwa ajili ya Msalaba huo. Jengo hili linaitwa Calvario na lilibarikiwa tarehe 14-1-2002. Parokia inafurahi kwamba Kardinali alikubali kuanza njia ya Msalaba wakati wa Ijumaa Kuu.

Sakrament na Ibada kwa Miaka 50 ya Parokia

Kufuatana na vitabu vyetu mpaka tarehe 13-1-2002 Parokia ilikuwaa na;-

Ubatizo	==	30002
Kipaimara	==	10998

Ndoa	==	2982
Ushemasi	==	3-Fr. Mbiku, Fr. Ndekero, Fr. Muba 4-7-1971
Upadrisho	==	1- Fr. Stephan Niliwila – 13-7-1975
Mazishi	==	6886

Miito

Mapdre wawili wazalendo walifanya Misa yao ya shukrani katika Parokia yetu kwa sababu familia zao walikuwa waamini katika Parokia ya Msimbazi. Padre Benedict Shayo ambaye alipewa daraja la Upadrisho mwaka 1992 aliadhimisha Misa ya Shukrani 17-1-1993. Familia ya Pdre Benedict ilikaa Vingugnguti, wakati huo Vingunguti ilikuwa Kigango cha Msimbazi. Padre Eusabius Nzigilwa ambaye alipewa daraja la Upadrisho mwaka 1995 aliadhimisha Misa ya shukrani Msimbazi tarehe 2-7-1995. Familia yake ilikaa Ilala Flats.

Tarehe 13-1-2002 Msimbazi ilikuwa haina Mafrateri wa Jimbo kutoka Parokiani katika Seminari zote kuu za Tanzania.

Ingawa Parokia ya Wakapuchini mpaka mwaka 2002 hakuna ndugu hata mmoja kutoka Parokia yetu ambaye amejiunga na shirika hili la Ki-Fransisko.

Staff tarehe 13-1-2002

Padre Mnsuetus Brikhof	==	Paroko
Padre Benedict Hema	==	Msaidizi
Padre Switbert Massao	==	Msaidizi
Bruda Andreas Mwanga	==	Msaidizi
Sista Getrud Kitira [Kilimanjaro]	==	Secetary